(١)

Ramadhani ni Mwezi wa kuepushwa na Moto.

Prof.Ayman Alasar

Sifa zote njema ni zake mwenyezi Mungu Mtukufu Mola wa viumbe vyote, anayesema katika Kitabu chake Kitakatifu:

{يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ}

{Enyi mlio amini! Mmeandikiwa Saumu, kama walivyoandikiwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mwenyezi Mungu}.

Na ninashuhudia kuwa hakuna Mungu mwingine aabudiwaye kwa haki sipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, peke yake hana mshirika wake. Na ninashuhudia kuwa Bwana wetu na Mtume wetu Muhammad ni Mja na Mjumbe wake. Anasema S.A.W: Mtu yoyote atakayeufunga Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa Imani na kwa kumtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu, basi atasamehewa madhambi yake aliyoyafanya. Ewe Mola wetu msalie na umbariki yeye na Jamaa zake na Maswahaba wake wote. Na mwenye kuwafuata kwa Wema mpaka siku ya Malipo.

Na baada ya utangulizi huu.

Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ameupa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani uliobarikiwa sifa Maalumu ya tunu ambazo hazipatikani katika miezi mingine, na miongoni mwazo ni kuwa kwake Mwezi wa Uongofu ambao ndani yake viliteremshwa vitabu vya Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambapo anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{شَهْرُ رَمَضَانَ الَّذِي أُنْزِلَ فِيهِ الْقُرْآنُ هُدًى لِلنَّاسِ وَبَيِّنَاتٍ مِنَ الْهُدَى وَالْفُرْقَانِ ..}

{Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'ani kuwa ni uwongofu kwa watu, na hoja zilizo wazi za uwongofu na upambanuzi}

Na anasema Mtume wetu S.A.W: Vitabu vya Ibahimu viliteremshwa ndani ya usiku wa Kwanza wa Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani, na Taurati nayo iliteremshwa siku sita za Mwezi Mtukufu wa ramadhani, na Injili ikateremshwa ndani ya siku ya kumi na tatu za mwezi mtukufu wa Ramadhani, na Zaburi ikateremshwa ndani ya siku kumi na nane za Ramadhani, nayo Qurani tukufu iliteremshwa ndani ya siku kumi na nne za mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Na miongoni mwa tunu hizo ni kwamba huu ni Mwezi wa Dua na Maombi, kwani Dua na Maombi ni katika mambo makubwa ya utiifu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kwa ajili ya njia mbalimbali za kujikurubisha kwake ambazo Mja huzitumia. Na Mzingativu yoyote wa Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu atakuta kwamba Aya ya Dua imekuja katikati ya Aya za Swaumu, ambapo anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ}

{Na waja wangu watakapo kuuliza khabari zangu, waambie kuwa Mimi nipo karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anapo niomba. Basi na waniitikie Mimi, na waniamini Mimi, ili wapate kuongoka}

Na katika hayo kuna ishara ya kwamba Dua ya Mfungaji ina nafasi kubwa zaidi ya kupokelewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Anasema

Mtume wetu S.A.W: Mwenye kufunga ana Dua zisizokataliwa. Na anasema Mtume S.A.W: Watu watatu Dua zao hazikataliwi. Kiongozi Mwadilifu, na Mwenye kufunga Pindi anapofuturu, na Dua ya mtu aliyedhulumiwa Mwenyezi Mungu Mtukufu huinyanyua juu ya mawingu, na milango ya mbingu hufunguliwa kwa ajili ya Dua hiyo. Na kisha Mwenyezi Mungu Mtukufu husema: Na kwa Utukufu wangu, nitakunusuru haka baada ya kupita muda mrefu.
Na huwenda katika sifa hizo Maalumu za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ameujaalia Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani kuwa ni mwezi wa Kuachiwa huru na Moto. Ambapo Mtume S.A.W anasema: Unapokuwa usiku wa Kwanza wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani Mashetani wote hufungwa pingu pamoja na Majini waovu, na Milango ya Moto hufungwa, na hakuna mlango wowote kati ya milango yake hiyo unaofunguliwa, na Milango yote ya Pepo hufunguliwa, na hakuna mlango wowote unaofungwa, na ataita mwenye kuota, akisea: Ewe mtafutaji wa heri njoo, na Ewe mtafutaji wa Shari sita hapo ulipo, na ana Mwenyezi Mungu Mtukufu atakaowaachia kutoka Motoni. Na anasema Mtume S.A.W: Hakika ana Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kila wakati wa kufuturu atakaowatoa Motoni. Na maana ya kutolewa Motoni ni kwamba wale ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu atawapa neema hii ya kuachwa huru na kutolewa Motoni, kamwe hawataingizwa Motoni.
Kwa hivyo, Swaumu ni mmoja kati ya milango ya heri, na ni mojawapo ya mambo yanayomkinga Mja wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na adhabu ya Moto. Na anasema Mtume S.A.W: Na Swaumu ni kinga kwa Maana ya kizuizi kinachomzuia Mja na Moto. Na anasema Mtume S.A.W: Hafungi Mja yoyote sikuoja kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu Isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu atauweka mbali na Moto uso wake kwa Swaumu hiyo, siku ya Kiama kwa umbali wa Miaka sabini.

Na kutoka kwa Muadh bin Jabal R.A amesema: Nilikuwa na Mtume S.A.W, safarini, na siku moja nikawa karibu yake na huku tunatembea, na nilipomwona akiwa katika hali ya kutokuwa na jambo lolote linalomshughulisha, nikamwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, hebu niambie ni amali gani itakayoniingiza Peponi na itakayonikinga na Moto, akasema: Hakika umeniuliza jambo kubwa sana. Na hakika jambo hili ni jepesi kwa yule aliyerahisishiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, Ni kumuabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu na usimshirikishe na kitu chochote, na ukasimamisha Swala tano, ukatoa Zaka, ukafunga Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ukahiji Nyumba Tukufu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kisha akasema: Je nikujulishe milango ya heri? Swaumu ni kinga, na Sadaka hufuta makosa, kama vile maji yanavyouzima moto...

Swaumu pia ni moja ya waombezi ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu anaukubali uombezi wao siku ya Kiama ambapo anasema Mtume S.A.W:  Swaumu na Qurani ni viombezi vya Mja siku ya Kiama. Swaumu itasema: Ewe Mola wangu, Mimi nimemzuia chakula na matamanio mchana kutwa basi nijaalie niwe mwombezi wake kwa idhini yako, na Qurani Tukufu itasema: mimi nimemzuia usingizi wa usiku basi nijaalie niwe mwombezi wake, akasema. Vikajaaliwa kuwa viombezi.

Swaumu pia ni moja kati ya sababu za kusamehewa, na  Madhambi ni moja kati ya njia za Peponi. Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaahidi waja wake wenye kufunga, Waumini wa kike na wa kiume Msamaha na Malipo makubwa, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{إِنَّ الْمُسْلِمِينَ وَالْمُسْلِمَاتِ وَالْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ وَالْقَانِتِينَ وَالْقَانِتَاتِ وَالصَّادِقِينَ وَالصَّادِقَاتِ وَالصَّابِرِينَ وَالصَّابِرَاتِ وَالْخَاشِعِينَ وَالْخَاشِعَاتِ وَالْمُتَصَدِّقِينَ

(٥)

وَالْمُتَصَدِّقَاتِ وَالصَّائِمِينَ وَالصَّائِمَاتِ وَالْحَافِظِينَ فُرُوجَهُمْ وَالْحَافِظَاتِ وَالذَّاكِرِينَ اللَّهَ كَثِيرًا وَالذَّاكِرَاتِ أَعَدَّ اللَّهُ لَهُم مَّغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا}

{Hakika Waislamu wanaume na Waislamu wanawake, na Waumini wanaume na Waumini wanawake, na wat'iifu wanaume na wat'iifu wanawake, na wasemao kweli wanaume na wanawake, na wanao subiri wanaume na wanawake, na wanyenyekevu wanaume na wanawake, na watoao sadaka wanaume na wanawake, na wanao funga wanaume na wanawake, na wanao jihifadhi tupu zao wanaume na wanawake, na wanao mdhukuru Mwenyezi Mungu kwa wingi wanaume na wanawake, Mwenyezi Mungu amewaandalia msamaha na ujira mkubwa}.

Na anasema Mtume S.A.W: Mtu yoyote atakayeufunga Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa Imani na kwa Kumtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu atasamehewa madhambi yake yote aliyoyafanya.
Na anasema Mtume S.A.W: Mtu yoyote atakayeswali Tarawehe ndani ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kwa Imani na kwa kumtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu, basi atasamehewa madhambi yake yote aliyoyafanya. Bali ndani ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kuna usiku mmoja, ambao atakayeruzukiwa kuuhuisha kwa ibada, na kwa kusoma Qurani Tukufu na kwa kuomba Dua, na akawafikishwa kumtii Mola wake Mtukufu ndani ya Usiku huo, basi Madhambi yake yatasamehewa.Na huo ni Usiku wa Cheo.
Na anasema Mtume S.A.W: Mtu yoyote atakayeswali Usiku wa Cheo kwa Imani na kwa kumtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu, atasamehewa makosa yake yote aliyoyafanya.
Na katika ufafanuzi mwingine ya kwamba swaumu ni moja ya njia za Peponi, anasema Mtume S.A.W: Hakika Peponi kuna chumba

ambacho kinaonekana kwa uwazi wake kwa ndani yake, Mwenyezi Mungu Mtukufu amekiandaa kwa yoyote atakayewalisha watu chakula, na akasema maneno mazuri yaliyo laini, na akaendelea na swaumu, na akaswali hali ya kuwa watu wamelala.
Na kutoka kwa Abuu Huraira R.A kwamba siku moja, Mtume S.A.W aliwauliza Maswahaba wake: Ni nani miongoni mwenu aliyeamka leo akiwa na swaumu? Abu Bakari akasema: Mimi. Mtume akauliza: Ni nani miongoni mwenu aliyemtembelea mgonjwa? Abu Bakari akasema: Mimi. Akasema Mtume S.A.W: Ni nani miongoni mwenu aliyeshuhudia Mazishi leo? Abu Bakari akasema: Mimi. Mtume akasema: Ni nani aliyemlisha masikini yoyote leo? Abu Bakari akasema: Mimi. Mtume S.A.W akasema: Hayakusanyiki Mambo haya yote kwa mtu mmoja ndani ya siku moja isipokuwa mtu huyo ataingia Peponi.
Na alipokuja Abu Amama Baahiliy R.A kwa Mtume S.AW, akamuuliza: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, niamrishe mimi ninfanye jambo ambalo litaniingiza Peponi, Mtume S.A.W akasema: Shikamana na Swaumu kwani Swaumu haina mfano wake.
Hakika ya Swaumu ni siri baina ya Mja na Mola wake na hakuna mtu yeyote mwenye uwezo wa kuujua ukweli wa siri hii, mwenye kufunga anaweza kuwa peke yake na hakuna anayemwona isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na ana uwezo wa kuyafanya yale aliyomyaharamishia Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa Swaumu, lakini hayafanyi, kwa kuwa anatambua fika tena kwa uhakika, kwamba ana Mola anayemwona katika kila jambo lake, na analiacha kwa kumwogopa Mwenyezi Mungu Mtukufu na adhabu yake, na kwa kutaka thawabu zake, na kwa kuamini kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu yuko pamoja naye. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

(٧)

{أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ مَا يَكُونُ مِنْ نَجْوَى ثَلَاثَةٍ إِلَّا هُوَ رَابِعُهُمْ وَلَا خَمْسَةٍ إِلَّا هُوَ سَادِسُهُمْ وَلَا أَدْنَى مِنْ ذَلِكَ وَلَا أَكْثَرَ إِلَّا هُوَ مَعَهُمْ أَيْنَ مَا كَانُوا ثُمَّ يُنَبِّئُهُمْ بِمَا عَمِلُوا يَوْمَ الْقِيَامَةِ إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ}

{Kwani huoni kwamba Mwenyezi Mungu anajua vilivyomo katika mbingu na vilivyomo katika ardhi? Hauwi mnong'ono wa watu watatu ila Yeye huwa ni wane wao, wala wa watano ila Yeye huwa ni wa sita wao. Wala wa wachache kuliko hao, wala walio wengi zaidi, ila Yeye yu pamoja nao popote pale walipo. Kisha Siku ya Kiyama atawaambia waliyo yatenda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu}.

Na Swaumu ni katika Ibada ambazo Mwenyezi Mungu Mtukufu amezipa daraja za juu, ambapo ameinasibisha Ibada hii ya Swaumu na Yeye, na akayafanya malipo yake kuwacni yake yeye Mtukufu, ambapo anasema Mtume S.A.W: Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: Matendo yote ya Mwanadamu ni yake isipokuwa Swaumu ni yangu na mimi ndiye ninayoilipa.
Na katika mapokezi mengine: Matendo yote ya Mwanadamu huongezeka, kila jema kwa kumi mfano wake, mpaka ongezeko la mia saba. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: Isipokuwa Swaumu, hakika ya Swaumu ni yangu mimi na mimi ndiye ninaeilipa. Kwa hiyo, Wanachuoni wanasema: Inatosha kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema: Swaumu ni yangu Mimi. Ni kuipa daraja la juu kuliko Ibada zingine zote. Na imesemwa kwamba: Hakika mambo yalivyo, ni kuwa nyongeza hiyo katika ibada ya Swaumu, ni kuwa katika Swaumu haabudiwi isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa Maana hiyo, Swaumu ni Ibada yenye nia takatifu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, haiingiliwi na ria. Na inasemwa pia

kwamba Swaumu ni Ibada ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu anaIpenda zaidi katika Ibada zote. Kwani mwenye Swaumu daima humwogopa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuichunga mipaka yake, na hupupia jinsi ya kuutumia vizuri Mwezi huu uliobarikiwa, na akajiweka yeye mwenyewe tayari kuzipokea Tuzo za Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani ya Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani, kwa matumaini ya kuwa miongoni mwa wale ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu atawaepusha na Moto.

Na ninaisema kauli yangu hii, na ninamwomba msamaha Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili yenu na kwa ajili yangu

*   *   *

Sifa zote njema ni zake mwenyezi Mungu Mtukufu Mlezi wa viumbe vyote. Na rehma na amani ziwe juu ya Mtume wa Mwisho katika Mitume, na Manabii wake Mwenyezi Mungu Mtukufu, Bwana wetu Muhammad S.A.W, na Jamaa zake, na Maswahaba wake wote, na atakayewafuata kwa Wema mpaka siku ya Malipo.

Ndugu zangu Waislamu.

Hakika ya Swaumu inayokuwa sababu ya kuepushwa na Moto ni ile inayomzuia Mfungaji na kila aina ya mwenendo mbaya, husimama kati yake na Maasi na humfanikishia uchamungu ambao ndilo lengo kuu na Matunda ٦a Swaumu. Mtu anatakiwa asile chochote cha Haramu, na wala asiingie katika kuvunja heshima za Watu, wala

asimshambulie mtu yoyote kwa maneno machafu, wala asitembee na usengenyaji baina ya watu, na asiushuhudie uzushi wowote, na asiseme isipokuwa yanayomridhia Mwenyezi Mungu Mtukufu, na asilipize ovu kwa ovu mfano wake; bali aliondoshe kwa jambo lililokuwa zuri zaidi, akiwa amejipamba na Tabia njema za wanaofunga. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{وَإِذَا سَمِعُوا اللَّغْوَ أَعْرَضُوا عَنْهُ}

{Na wanapo sikia upuuzi hujitenga nao}.

Na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{وَالَّذِينَ هُمْ عَنِ اللَّغْوِ مُعْرِضُونَ}

upuuzi ya mambo na hujiepusha ambao Na

Na anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{ادْفَعْ بِالَّتِي هي أحسن السيئة}

zaidi mema yaliyo kutenda kwa maovu Kinga

Na anasema Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu: Swaumu ni kinga, na mmoja wenu anapokuwa katika siku yake ya Swaumu basi asiseme maneno machafu na wala asifoke, na iwapo mtu atamtukana au akagombana naye basi na aseme: Hakika mimi ntu niliyefunga.
Na anasema Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, S.A.W: Swaumu sio kuacha kula na kunywa; bali Swaumu ni kuacha mambo ya kipuuzi na maneno machafu ... Na miongoni mwa sababu za kuepushwa na Moto ni Mwislamu kujiepusha na kumsengenya ndugu

yake ambaye hayupo. Na anasema Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, S.A.W: Na yoyote atakayejiepusha na kumsengenya ndugu yake, basi huyo atakuwa na haki kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu amuepushe na moto.

Hakika Mfungaji wa kweli anayenufaika na malipo ya Swaumu ni yule ambaye athari ya Swaumu huonekana katika mwenendo wake na jinsi anavyotangamana na watu, ambapo Swaumu humzoesha Mfungaji kujizuia na kuidhibiti nafsi yake na kuiongoza, mpaka ikafikia katika mambo yenye Kheri ndani yake na furaha Duniani na kesho Akhera. Kwani Nafsi kawaida yake ni kuamrisha mabaya isipokuwa nafsi chache alizozipa rehma Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na iwapo mtu ataiacha huru nafsi yake ifanye itakavyo, basi itamtumbukiza kwenye maangamizi. Na iwapo ataimiliki na kuidhibiti yeye mwenyewe, atakuwa amefanikiwa kuiongoza hadi daraja la juu la Wema na mazuri yatakiwayo, na haya hayawezi kupatikana isipokuwa kwa yule mwenye Swaumu ya kweli, mwenye kuuhisi Utukufu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Swaumu yake hiyo, huku tumbo lake, utupu wake, ulimi wake, na viungo vyake vyote vikiwa vimefunga na kujizuia na kila alichokiharamisha Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kama ambavyo Mfungaji wa kweli ni yule mwenye kuyaboresha matendo yake na kuyafanya kwa nia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na akashughulikia kupokelewa kwake, basi na tumuangalie kipenzi cha Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mtume Ibrahim A.S, anamwomba Mola wake amkubalie Maombi yake akiwa anatenda kazi nzuri na bora aliyoamrishwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu aifanye, na sio nyingine bali ni ujenzi wa Kaabah Tukufu. Na katika hilo anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

(١١)

{وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَاهِيمُ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ وَإِسْمَاعِيلُ رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّا إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ}.

ile ya misingi inyanyua walipo Ismail na Ibrahim kumbukeni Na Hakika !Tutakabalie !wetu Mlezi Mola Ewe :wakaomba Nyumba Mjuzi Msikizi ndiye Wewe

Na Bwana wetu S.A.W alikuwa anasema: kuweni kwa ajili ya kupokelewa matendo yenu ni wenye kutilia mkazo hima kutoka kwenu kwa kufanya kazi, kwani hamjamsikia Mwenyezi Mungu Mtukufu akisema:

{إِنَّمَا يَتَقَبَّلُ اللَّهُ مِنَ الْمُتَّقِينَ}.

Mwenyezi Mungu huwapokelea wachamngu.

Ewe Mola wetu tukaalie sisi tuwe katika wale utakaowaweka mbali na moto, na utujaalie sisi tuwe katika wale wenye kukubaliwa maombi yao.